

HALMASHAURI YA WILAYA MBEYA

***MUHTASARI WA TAAARIFA
YA UTEMDAJI KAZI NA
UWAJIBIKAJI WA
HALMASHAURI KWA
MWAKA WA FEDHA
2020/2021.***

UTANGULIZI:

1.1 MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA HALMASHAURI

- Kwa mwaka wa fedha 2020/2021 Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya ilipanga kukusanya na kutumia jumla ya **Tshs. 50,743,721,389.00**. Ikiwa, Mishahara **Tshs. 36,867,322,280.00**, Ruzuku toka Serikali Kuu na Wahisani **Tshs. 7,682,348,617.00**, **Tshs. 2,305,938,492.00** fedha za matumizi mengineyo (OC) na **Tshs. 3,388,212,000.00** Mapato ya ndani (Ikiwa mapato halisi ni **Tshs. 3,534,421,000.00** na mapato mengineyo ni **Tshs. 353,791,000.00**)

1.2 MAPOKEZI YA FEDHA

Katika kipindi cha 2020/2021, Halmashauri imeweza kukusanya jumla ya **Tshs. 41,539,338,693.00** sawa na 81.9% ya makadirio, ambapo mapato toka vyanzo vya ndani ni **Tshs. 4,061,865,273.00** sawa na 104% ya makadirio, Miradi ya Maendeleo **Tshs. 5,850,792,288.00** sawa na 76% ya makadirio, Mishahara **Tshs. 30,203,041,299.00** sawa na 82% na matumizi mengineyo (OC) **Tshs. 1,423,639,833.00** sawa na 62% ya makadirio.

1.3 UKUSANYAJI WA MAPATO YA NDANI

- Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiria kukusanya na kutumia jumla ya **Tshs. 3,888,212,000.00** kutoka vyanzo vya ndani (Own Source – Mapato halisi **Tsh. 3,534,421,000.00** na Mapato Mengineyo **Tsh. 353,791,000.00**). Jumla ya Makusanyo ya mapato ya ndani kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ni **Tshs. 4,061,865,273.00** sawa na **asilimia 104** kama inavyoonekana hapa Chini;-

Na	Mwaka	Bajeti ya mapato ya ndani	Fedha iliyokusanywa	%
1	2020/2021	3,888,212,000.00	4,061,865,273.00	104

1.3.1 CHANGAMOTO ZA UKUSANYAJI WA MAPATO YA NDANI

Halmashauri inakabiliwa na changamoto mbalimbali za ukusanyaji wa mapato ya ndani zikiwemo:

- 1.Kampuni au wafanyabiashara kutotoa takwimu sahihi za mauzo kwa ajili ya kukokotoa ushuru wa huduma.
- 2.Kushindwa kupata takwimu sahihi ya huduma iliyotolewa na minara ya simu iliyopo katika maeneo ya Halmashauri na hivyo kushindwa kukokotoa ushuru wa huduma.
- 3.Jiografia ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya kutawanyika hivyo kutumia gharama kubwa ya kuthibiti wakwepa ushuru wa Halmashauri.

1.3.2 MAFANIKIO YA HALMASHAURI

Halmashauri kupitia fedha za mapato ya ndani imeweza kuchangia Miradi mbalimbali ya Maendeleo ikiwemo

- i. Ununuzi wa gari kwa ajili ya shughuli za Halmashauri.
- ii. Ununuzi wa pikipiki 12 kwa ajili ya kusaidia ukusanyaji wa mapato.
- iii. Ununuzi wa mashine ya kufyatulia tofali kwenye jengo la Utawala.

2. UWEZESHWAJI WANANCHI KIUCHUMI

Katika kipindi cha mwaka 2020/2021, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya imetoa mikopo kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu wenye thamani ya **Tshs. 839,000,000.00**. ikiwa **Tshs. 344,000,000.00** fedha za mapato ya ndani na **Tshs. 495,000,000.00** ni fedha za marejesho ya mikopo ya nyuma (Revolving Fund).

3. UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA IDARA

1. IDARA YA MIPANGO, TAKWIMU NA UFUATILIAJI.

Katika kipindi cha mwaka 2020/2021 Idara ya Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji imetekeleza shughuli zifuatazo;

- ❖ Kuandaa mpango wa bajeti na matumizi kwa mwaka 2021/2022
- ❖ Kuratibu, kusimamia na kufuatilia shughuli zinazofadhiliwa na UNICEF
- ❖ Kuratibu na Kusimamia fedha za mfuko wa Jimbo
- ❖ Kufanya ufuatiliaji na tathimini ya miradi ya Maendeleo inayotekelezwa ngazi ya Kata/Kijiji.
- ❖ Kuandaa taarifa ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC)

2. IDARA YA UTUMISHI NA UTAWALA

Idara ya Utumishi na Utawala yenye jumla watumishi 3019 imetekeleza majukumu yafuatayo;

- ❖ Kusimamia na kufanya uchambuzi wa taarifa za watumishi.
- ❖ Kupandisha vyeo watumishi 1089
- ❖ Kuajiri watumishi wa Kada mbalimbali.
- ❖ Kutoa mafunzo kwa watumishi wa ajira mpya kwa kuzingatia taratibu za utumishi wa Umma.
- ❖ Kusimamia ulipwaji wa stahiki mbalimbali za watumishi.

3. IDARA ARDHI NA MALIASILI

Idara ya Ardhi na Maliasili imetekeleza kazi zifuatazo katika kipindi cha mwaka 2020/2021;

- ❖ Kupanga, kupima na kuandaa hati za maeneo mbalimbali
- ❖ Kuandaa Hati za umiliki Ardhi.
- ❖ Kushughulikia kero, malalamiko na migogoro ya Ardhi.
- ❖ Kufanya uthamini wa mali wa wananchi kwa ajili ya kulipa eneo la viwanda Mwakwenje na eneo la mradi wa kupanga lmezu.

4. IDARA YA UJENZI

Katika kipindi cha mwaka 2020/2021 Idara ya Ujenzi imefanya kazi ya kusimamia kazi za miradi mbalimbali inayotekelezwa ndani ya Halmashauri ikiwa ni pamoja na;

- ❖ Miradi iliyopata fedha za EP4R
- ❖ Ujenzi wa Jengo la Utawala.
- ❖ Ujenzi wa Wodi 3 Hospitali ya Wilaya Inyala

5. IDARA YA MIFUGO NA UVUVI

Katika kipindi cha mwaka 2020/2021 Idara ya Mifugo na Uvuvi imetekeleza shughuli zifuatazo;

- ❖ Kuendelea kufanya ukarabati wa miundombinu ya mifugo kama vile majosho.
- ❖ Kudhibiti magonjwa ya mifugo yanayoenezwa kwa kupe na wadudu wengine.
- ❖ Kusimamia uogeshaji wa unyunyiziaji dawa mifugo
- ❖ Kutoa chanjo dhidi ya maradhi mbalimbali ya mifugo

6. IDARA YA MAENDELEO YA JAMII

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021, Idara ya Maendeleo ya Jamii ilitekeleza majukumu yafuatayo;

- ❖ Kufanya tathmini na kutoa mafunzo kwa vikundi vya wanawake, vijana na walemavu waliomba mikopo.
- ❖ Kufanya maandalizi na kutoa mikopo ya kiasi cha **Tshs. 839,000,000.00** kwa vikundi 54. vikundi 27 vya Wanawake kiasi cha **Tshs. 237,550,000.00** na Vikundi 25 vya Vijana kiasi cha **Tshs. 592,450,000.00** na vikundi vya watu wenye ulemavu 2 kiasi cha **Tshs. 9,000,000.00**

7. IDARA YA ELIMU SEKONDARI

Idara ya Elimu Sekondari katika kipindi cha mwaka wa 2020/2021 imeongeza ufaulu wa wanafunzi na kuboresha mazingira ya kufundishia kwa kusimamia ujenzi wa vyumba vya madarasa, matundu ya vyoo na maabara katika shule zilizopata fedha toka vyanzo mbalimbali vya mapato, ambapo ufaulu wa matokeo ya kidato cha nne umeongezeka kutoka **asilimia 88.77** kwa mwaka 2019 hadi kufikia **asilimia 88.8** kwa mwaka 2020 ikiwa wanafunzi waliofanya mtihani huo walikuwa 3769 na waliofaulu ni wanafunzi **3346** sawa na **asilimia 88.8** na wanafunzi **423** walifeli sawa na **asilimia 11.2**. Aidha, jitihada na mikakati mbalimbali ilifanyika katika kuhakikisha malengo yaliyowekwa na Halmashauri ya Wilaya yanatimia.

8. IDARA YA FEDHA

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 imetekeleza shughuli mbalimbali ikiwemo;

- ❖ Kusimamia shughuli za ukusanyaji wa mapato ya ndani ya Halmashauri
- ❖ Kuandaa taarifa za mwisho za Hesabu kwa mdhibiti na mkaguzi wa Hesabu za mwaka.
- ❖ Kuandaa na kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Bunge ya Serikali za Mitaa (LAAC)

9. IDARA YA KILIMO

Idara ya Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika imetekeleza majukumu yafuatayo katika kipindi cha mwaka 2020/2021;

- ❖ Kuanzisha mashamba darasa kwa ajili ya kutoa elimu kwa wakulima.
- ❖ Kufanya ukaguzi wa maduka ya wauza pembejeo za kilimo.
- ❖ Kusimamia ujenzi wa vitalu nyumba.
- ❖ Kusimamia usafi wa skimu za umwagiliaji

10. IDARA YA AFYA.

Katika kipindi cha mwaka 2020/2021 Idara ya Afya imetekeleza shughuli zifuatazo;

- ❖ Kufanya usimamizi shirikishi katika Vituo tiba ili kuboresha huduma za Afya
- ❖ Kufanya usambazaji wa dawa, vifaa tiba na Gesi katika vituo vya tiba.
- ❖ Kufanya Rufaa za wagonjwa toka Zahanati, Vituo vya Afya kwenda Hospitali Teule ya Wilaya - Mbalizi.
- ❖ Kufanya ufuatiliaji wa utoaji wa huduma za Afya katika Vituo vya Afya na Zahanati.

11. IDARA YA ELIMU MSINGI

Katika kipindi cha mwaka 2020/2021 Idara ya Elimu Msingi imetekeleza shughuli zifuatazo;

- ❖ Kuratibu na kusimamia ajira za walimu wapya waliopangiwa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya.
- ❖ Kufanya ufuatiliaji na tathmini shughuli za ukusanyaji wa takwimu za miundombinu kwa kutumia mfumo wa BEMIS
- ❖ Kusimamia zoezi la usajili wa wanafunzi kwenye mfumo wa Prem kwa elimu ya awali hadi darasa la VII
- ❖ Kupokea na kugawa vitabu vya kiada vya darasa la VII.

12. KITENGO CHA MANUNUZI

Kitengo cha Manunuzi katika kipindi cha mwaka 2020/2021 kimeteteleza shughuli zifuatazo;

- ❖ Kuandaa mpango wa manunuzi wa mwaka.
- ❖ Kutekeleza mpango wa manunuzi wa mwaka.
- ❖ Kuwezesha Idara/Vitengo kupata huduma ya manunuzi.
- ❖ Kuingiza taarifa za manunuzi kwenye mfumo wa PROCUREMENT MANAGEMENT INFORMATION SYSTEM (PMIS)
- ❖ Ununuzi wa vifaa vya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya Inyala na jengo la Utawala.

13. KITENGO CHA SHERIA

Katika mwaka wa fedha 2020/2021 Kitengo cha Sheria kimeteteleza majukumu yafuatayo;

- ❖ Kutoa ushauri kwa Menejimenti katika masuala ya kisheria.
- ❖ Kusimamia mashauri (kesi) katika mahakama mbalimbali.
- ❖ Kuandaa/kufanya upekuzi (vetting) wa mikataba ya ujenzi.
- ❖ Kutoa mafunzo na kuapisha mabaraza ya Kata.
- ❖ Kuandaa rasimu ya taratibu za uendeshaji wa Serikali ya Kijiji pamoja na Sheria Ndogo za Halmashauri ya Kijiji.

14. KITENGO CHA UKAGUZI WA NDANI.

Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani kwa mwaka 2020/2021 kimefanya kazi zifuatazo;

- ❖ Kukagua mapato na matumizi kwa Akaunti zote za Halmashauri.
- ❖ Kukagua thamani ya fedha kwenye miradi ya ujenzi inayotekelezwa na Halmashauri.
- ❖ Kufanya ukaguzi maalum ujenzi wa madarasa Shule za Msingi
- ❖ Kufanya ukaguzi wa mfumo wa mapato.

15. KITENGO CHA MAZINGIRA NA UDHIBITI WA TAKA NGUMU.

Kitengo kimetokeleza majukumu yafuatayo;

- ❖ Kusimamia usafi na kusomba taka ngumu katika maeneo ya Mbalizi, Inyala, Itewe, Igoma na Songwe.
- ❖ Kusimamia shughuli ya kusawazisha na kusogeza taka ngumu katika dambo kuu la Shigamba.
- ❖ Kufanya ufatiliaji katika maeneo ya masoko na kiwanda cha Mbalizi Plastic.

16. KITENGO CHA UCHAGUZI.

Katika kipindi cha mwaka 2020/2021 Kitengo cha Uchaguzi kimeteteleza shughuli zifuatazo;

- ❖ Kufanya uhakiki wa vifaa vya uchaguzi mkuu.
- ❖ Kusimamia shughuli za uchaguzi mkuu wa Oktoba, 2020.
- ❖ Kusimamia uchaguzi mdogo wa udiwani Kata ya Iwiji.

17. KITENGO CHA TEHAMA

Ifuatayo ni taarifa ya utekelezaji wa Kitengo cha Tehama kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

- ❖ Kuifahamisha na kuielimisha jamii juu ya mambo yanayotekelezwa na Halmashauri kupitia vyombo mbalimbali vya habari.
- ❖ Kuhuisha na Kusimamia tovuti na kurasa rasmi za mitandao ya kijamii ya Halmashauri.
- ❖ Kutoa mafunzo, kuhuisha na kukagua mashine za kielektroniki za kukusanyia mapato (POS)

18. KITENGO CHA NYUKI.

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021, Kitengo cha Nyuki kilitekeleza shughuli zifuatazo;

- ❖ Kufanya ukaguzi wa manzuki katika vikundi mbalimbali vya wafugaji wa nyuki.
- ❖ Kusimamia uanzishwaji wa shamba darasa la ufugaji nyuki wadogo.
- ❖ Kusimamia utengenezaji wa mizinga ya wananchi
- ❖ Kutoa mafunzo ya ufugaji nyuki katika vikundi.

4. MIRADI YA MAENDELEO ILİYOTEKELEZWA NA HALMASHAURI KWA MWAKA 2020/2021.

Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya katika kipindi cha mwaka 2020/2021 imepokea kiasi cha **Tshs. 7,798,974,189.14** toka vyanzo mbalimbali, ikiwa ni kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Ambapo kiasi cha **Tshs. 5,963,980,286.26** ni fedha za Ruzuku ya Miradi ya Maendeleo, na kiasi cha **Tshs. 199,986,686.00** fedha zilizokuja nje ya bajeti na **Tshs. 1,635,007,216.85** ni fedha za mapato ya ndani ya Halmashauri kwa utekelezaji wa miradi ya Maendeleo kama unavyoonekana hapa chini.

1. FEDHA ZA COVID Tshs. 132,800,000/-

Halmashauri ya Wilaya Mbeya ilipokea jumla ya **Tshs. 132,800,000.00** toka kwa Wahisani kwa ajili ya kusaidia ujenzi wa vyumba vipya 4 vya madarasa na matundu 53 ya vyoo katika shule za Msingi Holongo, Nsenga, Sayuma na Isonso. Ujenzi wa vyumba vya madarasa umekamilika na ujenzi wa vyoo upo hatua ya umaliziaji.

2. SHULE ZA MSINGI ZILIZOPATA FEDHA ZA EP4R JUMLA YA Tshs. 160,000,000.00

a). Ujenzi wa vyumba viwili
vya madarasa shule ya
Msingi Mtakuja Tshs.
40,000,000/-

SHULE YA MSINGI ITALAZYA

b). Ujenzi wa vyumba viwili vya
madarasa shule ya Msingi
Italazya Tshs. 40,000,000/-

SHULE YA MSINGI PIPELINE

c). Ujenzi wa vyumba viwili vya
madarasa shule ya Msingi
Pipeline Tshs. 40,000,000/-

SHULE YA MSINGI MAPAMBANO

- d). Ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa shule ya Msingi Mapambano Tshs. 40,000,000/-

3. SHULE ZA SEKONDARI ZILIZOPATA FEDHA ZA MAABARA

Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya ilipokea **Tshs.**

210,000,000/- toka Serikali Kuu kwa ajili ya ujenzi wa maabara za sayansi katika shule za J/Usongwe, Sasyaka, Swaya na Iwiji.

a). Shule ya Sekondari Juhudi Usongwe Tshs. 60,000,000/-



4. UJENZI WA JENGO LA UTAWALA

- Ujenzi wa jengo la utawala upo katika hatua ya kuweka zege kwenye nguzo, mradi huu ulipata **Tshs 1,000,000,000/-** toka Serikali Kuu.



5. UJENZI WA ZAHANATI IZUMBWE I

- Mradi ulipata Tshs 80,000,000/- toka Serikali Kuu. Ujenzi upo katika hatua ya ukamilishaji kwenye baadhi ya majengo.



6. UJENZI WA WODI 3 HOSPITALI YA WILAYA INYALA

- Mradi wa ujenzi wa wodi tatu Hospitali ya Wilaya ulipata **Tshs. 500,000,000/-** toka Serikali Kuu. Ujenzi upo hatua ya kujenga tofari juu ya bimu na kuweka bimu kwenye wodi ya wanaume.



Ujenzi wa Kichomea Taka na Njia za kuunganisha majengo(Tshs.300,000,000)



Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa shule ya msingi Swaya.(Tshs.47,700,000)



Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa Shule ya msingi Utengule Usongwewe.(Tshs.40,000,000)



Ujenzi wa vyumba 3 vya madarasa, ofisi 1 na matundu 6 ya vyoo Shule ya Msingi Jitegemee (Tshs. 66,600,000)



Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa, ofisi 1 na matundu 7 ya vyoo Shule ya Msingi Mkombozi (Tshs. 47,700,000)



Ujenzi wa vyumba 2 vya Madarasa katika Shule ya Msingi Ilembo(Tshs.40,000,000)



Ujenzi wa vyumba 2 vya Madarasa katika Shule ya Msingi Songwe II(Tshs.40,000,000)



Ujenzi wa vyumba 3 vya madarasa na matundu 13 ya vyoo Shule ya Msingi Mapelele(Tshs.66,600,000)



Ujenzi wa vyumba 3 vya madarasa, ofisi 1, Madawati 60 na matundu 21 ya vyoo Shule ya Msingi Jojo (Tshs.66,600,000)



Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa na ofisi moja shule ya sekondari Malama(Tshs.41,670,000)



Ujenzi wa vyumba 9 vya madarasa Shule ya sekondari Juhudi Usongwwe (Tshs.110,000,000)



Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa na ofisi 1 shule ya sekondari Songwe (Tshs.20,000,000)



Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa na Ofisi 1 shule sekondari Ilembo (Tshs.40,000,000)



Mashine ya ndani ya Jengo la Kuchomea taka Hospitali ya Wilaya.



Vitalu 5 vya Miche bora ya Kahawa kata za Isuto,Igale na Iwindi(Tshs.8,000,000)



Utoaji wa mikopo vikundi vya Vijana,Wanawake na Watu wenye ulemavu (Tshs.230,000,000)



Kikundi cha Ulamsho toka Utengule usongwe mradi wa Kilimo(Tshs.10,000,000)



TASAF III

katika kipindi cha Julai hadi Disemba, 2020
Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya ilipokea
fedha za walengwa kiasi cha Shilingi
440,312,000 na kiasi cha Shilingi
438,400,000 zililipwa kwa walengwa 7,611
kati ya walengwa 7,646.

TASAF III CONT.....

Baadhi ya vifaa vilivyogawiwa kwa watoto wa walengwa wa Tasaf III



MAZINGIRA

Katika kipindi cha julai hadi Disemba, 2020 Halmashauri imefanya usafi wa mazingira kwa kuzoa taka ngumu wastani wa tani 22,200 katika Mamlaka ya Mji mdogo wa mbalizi ,Kata za Songwe, Inyala, Itewe na Igoma.





*AHSANTENI KWA
KUNISIKILIZA.*